# JARIDA LA USHIRIKA

ISSN 2714 - 2175 | Toleo Na: 011 | Julai - Septemba, 2022

AJENDA 10/30
KILIMO NI BIASHARA




## WAZIRI BASHE AZINDUA KAMISHENI YA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA





*"Ushirika – Pamoja Tujenge Uchumi"*

## YALIYOMO


| | |
|---|---|
| KUTOKA KWA MRAJIS | 02 |
| WAZIRI BASHE AZINDUA KAMISHENI YA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA | 03 |
| USHIRIKA NINA UHAKIKA UKO SALAMA - WAZIRI MKUU | 04 |
| MRAJIS AELEZEA MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA NA MWELEKEO WA BAJETI YA TCDC KWA MWAKA 2022/2023 | 05 |
| SPIKA WA BUNGE AZINDUA JENGO LA CHAMA CHA USHIRIKA LULU SACCOS | 06 |
| MCHAKATO WA UANZISHWAJI BENKI YA USHIRIKA UFANYIKE MAPEMA - DKT. ISHENGOMA | 07 |
| WANAHISA KCBL WATAKIWA KUONGEZA UWEKEZAJI | 08 |
| TCDC KUIMARISHA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA SACCOS | 09 |
| ELCT ND SACCOS KUZINDUA MATUMIZI YA KADI ZA 'ATM NA MOBILE BANKING' | 10 |
| VYAMA VYA USHIRIKA KUSAJILIWA KIDIGITALI | 11 |
| KAMATI YA KITAIFA YA KURATIBU HARAMBEE YA UJENZI WA ENEO LA MRADI WA KIWANDA CHA WANAWAKE YAZINDULIWA | 12 |
| CHAMA CHA USHIRIKA CHAANZISHA KIWANDA CHA KUSINDIKA MAFUTA YA ALIZETI | 14 |
| TUNDURU WAKUSANYA UFUTA TANI 2,300 KUPITIA STAKABADHI GHALANI | 15 |
| VYAMA VIKUU VYA USHIRIKA VYA MIKOA YA SHINYANGA NA GEITA VYAISHUKURU SERIKALI KUFUFUA VIWANDA VYA PAMBA | 16 |
| USHIRIKI WA TCDC KATIKA MAONESHO YA BIASHARA YA AFRIKA MASHARIKI | 17 |
| TCDC YASHIRIKI MAONESHO YA 46 YA KIMATAIFA YA BIASHARA | 18 |
| MAFANIKIO YA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA CHA KAHAMA (KACU) | 19 |
| HAI RURAL TEACHERS SACCOS WATOA MISAADA KWA KITUO CHA WATOTO CHA NEEMA | 22 |
| VYAMA VYA USHIRIKA MKOANI DODOMA VYATOA MISAADA | 23 |

## KUTOKA KWA MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA NA MTENDAJI MKUU WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

**Ndugu Wasomaji,**
Niwakaribishe tena katika Jarida la Ushirika, Toleo la 11, ambalo ni mfululizo wa majarida yanayoandaliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania katika jitihada za kuelimisha na kuhamasisha masuala na hatua mbalimbali zinazofanyika katika Sekta ya Ushirika.



*Dkt. Benson Ndiege, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).*

MCHANGO WA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA KUKUZA PATO LA TAIFA

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ni Taasisi ya Serikali inayojitegemea iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo ambayo ilianzishwa kwa mujibu wa sheria ya Vyama vya Ushirika Na 6 ya Mwaka 2013 ikiwa na jukumu la Kusimamia na Kuhamasisha Maendeleo ya Sekta ya Ushirika nchini, kama ilivyoanishwa katika kifungu cha 8 (l) cha sheria hiyo.

Tume inasimamia jumla ya vyama vya Ushirika 7,205 ambavyo vinatokana na Sekta mbalimbali zikiwemo za Kilimo, Mifugo, Madini, Fedha, Uvuvi na Nyumba. Wanachama wa Vyama hivyo ni Wafanyabiashara Wadogo na Wakati, ambao idadi yake ni jumla ya Watanzania milioni 12.

Aidha, Tume kama mdhibiti wa Sekta, inatoa msaada wa Kiusimamizi katika maeneo mbalimbali ya kitaalam kama vile Utendaji Kazi, Uzingatiwaji wa Sheria, Mifumo, Menejimenti ya Rasilimali Watu kwa kuhakikisha Vyama vina watumishi sahihi na wenye sifa.

Tume katika kutekeleza majukumu yake imefanikiwa kuratibu na kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini (MUVU) ambao unasaidia kuboresha utendaji kazi wa Tume, Vyama vya Ushirika pamoja na wadau wengine kwa ujumla.

Tume kupitia Ushirika imefanikiwa kuboresha maisha ya wananchi kupitia shughuli wanazozifanya zinazowaingizia kipato kwa muunganiko wa Ushirika. Kwa mfano, wakulima wameweza kulipwa fedha zao za mazao kwa uharaka baada ya kuuza mazao yao kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Tume imeendelea kufanya Usimamizi thabiti wa Vyama vya Ushirika ambao umechangia kwa kiasi kikubwa katika ongezeko la Pato la Taifa na kwa mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022 jumla ya Tani 9,804,347 za mazao ya kimkakati ziliuzwa kupitia Vyama vya Ushirika, na hivyo jumla ya Shilingi 2,917,816,152,983.61 zililipwa kwa wakulima.

Na Serikali imepata tozo za kodi mbalimbali kupitia Mamlaka zake zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfano, Serikali katika mwaka 2021/2022 ilipokea jumla ya Shilingi 15,144,077,319.16 zikiwa ni fedha za ushuru unaotokana na zao la Korosho uliolipwa na vyama vya TANECU, MAMCU, RUNALI, LINDI MWAMBAO, TAMCU na CORECU; Vilevile, jumla ya Shilingi 1,041,957,051.00 zimepokelewa kama ushuru katoka katika Vyama vya Ushirika vya KDCU na KCU kupitia zao la Kahawa.

Viwanda Vidogo, vya Kati na Vikubwa 279 vimeanzishwa nchini kupitia Mfumo wa Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika. Katika Msimu wa 2022/2023 Vyama Vya Ushirika vilitumia jumla ya Shillingi 397,706,245,786 kununua pembejeo za kilimo kwa ajili ya wakulima wa zao la Korosho, Kahawa, Tumbaku na Pamba.

Tume kupitia Vyama vya Ushirika imeendelea kuratibu masoko na biashara ya zao la Ufuta nchini ambapo katika Msimu wa 2022/2023 jumla ya kilo 79,170,426 zenye thamani ya Shilingi 245,130,400,328 zimeuzwa kupitia Ushirika katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani na Songwe na kuwezesha Halmashauri zake kupata Ushuru wa zao wenye thamani ya Shilling 6,022,450,313.

Tume vilevile inasimamia Vyama vya Ushirika vya Kifedha (SACCOS) ambapo hadi kufikia mwaka 2021 kabla ya kuanza kutekeleza Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha kulikuwa na SACCOS 3,831 zenye thamani ya Shilingi trilioni 1.6 na Akiba ya Shilingi bilioni 803 pamoja na Amana za Shilingi bilioni 149.2. Baada ya usajili mpya kwa mujibu wa Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha, hadi kufikia mwezi Novemba, 2022 kuna jumla ya SACCOS 743 zenye wanachama 1,731,237 wenye Amana za Shilingi bilioni 713.6, Mali za Shilingi bilioni 945.3 na Hisa zenye thamani ya Shilingi bilioni 149.2.

Kutokana na mafanikio yanayopatikana, Vyama vya Ushirika chini ya usimamizi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika vinafanya kazi nzuri ya kukuza uchumi wa wananchi. Hivyo, Watanzania walioko katika sekta zote wanahimizwa kujiunga katika Vyama vya Ushirika ili waweze kuinua uchumi wao na wa Taifa kwa ujumla.





## WAZIRI BASHE AZINDUA KAMISHENI YA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussen Bashe, amezindua Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), uzinduzi ambao umefanyika katika Ukumbi wa Kilimo 4 Jijini Dodoma.




*Makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), wakiwa katika picha ya pamoja na Menejmenti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika*

Kwenye uzinduzi huo Waziri Bashe amewataka Makamishina kuibadilisha TCDC na kuifanya iwe ya kibiashara zaidi ikiwa inaendelea kutoa huduma kama kawaida.

"Tume wamekuwa ni watu wa kutoa huduma bila kuangalia fursa zilizopo na wanazozisimamia ambazo nataka Makamishna mtumie fursa hizo kuifanya Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuwa ni sehemu ya manufaa na fada kwa Wanaushirika," alisema Mhe. Bashe.

Pia aliwasisitiza kufanya kazi na Menejementi ya Tume kwa kufuata misingi ya uwazi na uadilifu ili kuweza kuifanya Tume kuwa ni kimbilio la watu wote kwasababu Ushirika upo kila sehemu.

"Ni jukumu letu sote kumfanya Mkulima kupata faida ya kilimo chake na ni jukumu letu sote kuhakikisha kila mkulima au mwanaushirika yeyote anakuwa na imani na Tume ya Maendeleo ya Ushirikia Tanzania," alisema Mhe. Bashe

Waziri Bashe alisema kuwa wananchi wamekuwa na fikira ambazo si sahihi kuhusu Ushirika, sasa ni jukumu la Makamishna na Menejimenti ya Tume kuondoa hizo fikira mbaya kuhusu Ushirika, kwakuwa Ushirika wa leo si Ushirika wa enzi zile.

Naye Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Bw. AbdulMajid Nsekela alimhakikishia Waziri Bashe kuwa watafanya kazi kwa ushirikiano na Menejimenti ya Tume hatua kwa hatua.

Bw. Nsekela alisema kuwa Bodi itasimamia Tume vyema na Ushirika kwa ujumla na kuhakikisha wanawafanya wananchi walio nje ya Ushirika kutamani kujiunga katika Ushirika kama fursa za kujipatia vipato.

"Ndani ya miaka mitatu tutaacha alama na tutaanza na kufanya mabadiliko ya mtu mmoja mmoja na pia tutashirikiana na wadau wengine katika utendaji kazi zetu na tutaisimamia vizuri Tume ya Maendeleo ya Ushirikia Tanzania.



*Makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), wakiwa katika kikao cha uzinduzi wa Bodi ya Kamisheni ya Tume hiyo.*

## USHIRIKA NINA UHAKIKA UKO SALAMA - WAZIRI MKUU

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, ameipongeza Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa jitihada zake za kuhakikisha Ushirika unastawi na kuwa sehemu sahihi na salama ya uwekezaji wa mali za wanaushirika na wadau wengine ikiwa ni pamoja na kuinua uchumi wa mwanachama na Taifa kwa ujumla.



*Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, akizungumza na Wanaushirika kwenye Maonesho ya Nanenane, Jijini Mbeya*

"Naipongeza Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa jitihada zake za kuhakikisha Ushirika unastawi na kuwa sehemu sahihi na salama ya uwekezaji wa mali za wanaushirika na wadau wengine ikiwa ni pamoja na kuinua uchumi wa mwanachama mmoja mmoja na pato la Taifa; Nina uhakika Ushirika uko salama," amesema Waziri Mkuu.

Ametoa pongezi hizo tarehe 03/08/2022, alipofanya ziara ya kutembelea 'Kijiji cha Ushirika kwenye Maonesho na Maadhimisho ya NANENANE Kitaifa, yaliyofanyika kwenye viwanja vya John Mwakangale, Jijini Mbeya.

Katika msafara wake, Mhe. Waziri Mkuu aliambatana na viongozi mbalimbali wa Serikali, akiwemo Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Akson na Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. Anthony Mavunde.

Mhe. Majaliwa ameiagiza TCDC kuendelea kusimamia na kuhamasisha Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ya Ushirika na kusisitiza wadau washiriki kuhamasisha Vyama vya Ushirika, wanachama wa Vyama vya Ushirika na wadau wengine kuwekeza kupitia Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) kwa kununua hisa ili kufanikisha adhma ya Serikali ya kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika.




*Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, akisalimiana na viongozi alipotembelea "Kijiji cha Ushirika" kwenye maonesho ya Nanenane*



*Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, akiwa katika banda la Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania*



## MRAJIS AELEZEA MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA NA MWELEKEO WA BAJETI YA TCDC KWA MWAKA 2022/2023

Dhamira ya Serikali ni kutumia mfumo wa ushirika katika kuwezesha wananchi kiuchumi na kuchangia ipasavyo katika ustawi wao na wa Taifa kwa ujumla.

Akizungumza na waandishi wa habari Jijini Mbeya Mrajisi wa vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo Vya Ushirika Nchini, Drk Benson Ndiege amesema kazi kubwa ya Serikali ni kuhakikisha Ushirika unahamasishwa miongoni mwa watanzania na kusimamiwa kwa mujibu wa sheria ili kuwalinda na kuwanufaisha Wanaushirika.

Katika mwaka 2021/22, vipaumbele vya utekelezaji vilikuwa ni kuimarisha Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika, kuratibu Uhamasishaji, Utafiti na Utoaji wa Elimu ya Maendeleo ya Ushirika, kuimarisha Masoko, Uwekezaji na Uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Kuongezeka kwa uwekezaji katika Vyama vya Ushirika kumesababisha ongezeko la ajira kutoka 100,100 mwaka 2020/2021 hadi 146,555 mwaka 2021/2022. Kati ya ajira zilizopatikana, za kudumu ni 31,819, za mkataba ni 28,990 na za msimu ni 85,746.

Aidha, Tume imeanzisha matumizi ya Mfumo wa Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na kuhamasisha, kuratibu na kusimamia ujenzi na ufufuaji wa viwanda vya kati ili kuongeza thamani ya mazao;

Kuratibu na kuhamasisha ujenzi wa maghala ya mazao ya kilimo ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno, kuongeza thamani ya mazao na kuimarisha mfumo wa minada ya mazao yanayozalishwa na wananchi; na

Kutengeneza utaratibu wa uwezeshwaji vyama vya Ushirika (cooperative facilitation scheme) ili kuongeza ufanisi wa vyama vya Ushirika.



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, akizungumza katika Mkutano wa Waandishi wa Habari. Kulia ni Kaimu Naibu Mrajis -Uhamasishaji, Consolata Kiluma*

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Tume inaratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ili kuchochea maendeleo ya Ushirika nchini; Kufanya uthamini wa mali zinazomilikiwa na Vyama vya Ushirika kwa lengo la kutambua thamani halisi ya soko la mali hizo na hivyo kuviwezesha Vyama kufanya uwekezaji wenye tija.

Katika kuimarisha Udhibiti na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika, Tume katika mwaka wa fedha 2022/2023 inaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika, kukagua vyama vyote, na kuendelea kununua vitendea kazi ikiwemo ununuzi wa magari kwa ajili ya kuongeza tija kwa Maafisa Ushirika.

Tume vilevile imepanga kuanzisha Mfuko wa Bima ya Akiba na Amana za SACCOS utakaotumika kama kinga ya Akiba na Amana za wanachama wa SACCOS ambao SACCOS zao zitashindwa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria.

## SPIKA WA BUNGE AZINDUA JENGO LA CHAMA CHA USHIRIKA LULU SACCOS

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson, tarehe 5 Agosti, 2022 alizindua jengo la Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) cha LULU, Jijini Mbeya.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Jengo hilo, Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge aliwapongeza Wanaushirika wa LULU SACCOS kwa hatuakubwa ya Chama cha Ushirika kumiliki jengo lake.

"Nasikia faraja sana kuona vitu vizuri kama hivi vinafanyika Mbeya kiukweli LULU SACCOS mnatuheshimisha wanambeya na niwaambie tu hili jambo mlilofanya ni kubwa sana na muendelee kufanya mazuri na makubwa zaidi ya hili" amesema Spika wa Bunge




*Jengo la LULU SACCOS lililozinduliwa na Spika wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Tulia Ackson.*

Aidha, Mhe. Spika ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kuendelea kuvisimamia na kuvishauri ipasavyo Vyama vinavyofanya maendeleo kama ya LULU SACCOS kwani chama kama hicho kinahitaji ulezi na uangalizi wa karibu.

Vile vile Mhe. Spika amewataka LULU SACCOS kuendelea kuwa Chama bora cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kwa mkoa wa Mbeya na Taifa kwa ujumla na kuwahudumia wanachama wao kwa kufuata sheria za ushirika.



*Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson, akizungumza kwenye ufunguzi wa jengo la LULU SACCOS.*

Akizungumza katika uzinduzi wa jengo hilo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege ameahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa LULU SACCOS na Vyama vyote vya Ushirika vinavyoshiriki kwenye kujiletea Maendeleo.

"Tunahitaji kuwa na SACCOS ambazo zinaweza kufanya mambo ya maendeleo na makubwa kama haya kwa lengo la kuzidi kujiimarisha kiuchumi, nitoe wito kwa Vyama vingine vya Akiba na Mikopo kuwa na maono ya mbali ili wajiimarishe kiuchumi," alisema Dkt. Ndiege.

LULU SACCOS inatarajiwa kutoa Gawio la Hisa za umiliki wa jengo hilo ili kuwapa hamasa wanachama wake na kuchangia katika Pato la Taifa kupitia kodi ya zuio itakayotokana na malipo ya pango la ofisi.

Vilevile, Mapato kutokana na jengo hilo yataimarisha zaidi mtaji wa ndani ili kutokuwa wategemezi katika kuendesha shughuli za chama na kuimarisha utolewaji wa huduma kwa wanachama na jamii inayowazunguka na kuziboresha ziwe za kisasa zaidi.



*Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson (aliyesimama kulia) na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege (aliyesimama kushoto) wakati wa ufunguzi wa LULU SACCOS.*



*Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Tulia Ackson (aliyekaa katikati) na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege (wa pili kutoka kulia) wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi na watendaji waliohudhuria uzinduzi wa jengo la LULU SACCOS.*

## MCHAKATO WA UANZISHWAJI BENKI YA USHIRIKA UFANYIKE MAPEMA - DKT. ISHENGOMA

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Kilimo, Ufugaji na Maji, Mhe. Dkt. Christine Ishengoma amesema ili kuongeza tija kwenye Ushirika ni vyema mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Ushirika ukafanyika mapema iwezekanavyo kwa kuwa wazo la kuanzisha Benki ya Ushirika ni la Wanaushirika wenyewe, hivyo kukamilisha mchakato huu ni muhimu.

Dkt. Ishengoma ameyasema hayo alipokuwa akifunga Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani lililofanyika tarehe 1 Julai 2022 Mjini Tabora.

"Kwakuwa Serikali imeonyesha nia njema ya kuhakikisha adhma hii ya uanzishaji wa Benki ya Kitaifa ya Ushirika inakamilika; napenda kutoa wito wangu kwenu Wanaushirika, kununua Hisa katika Benki hii ya Ushirika," alisema.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mhe. Dkt. Christine Ishengoma, akizungumza katika Kongamano la Siku ya Ushirika Duniani.*

"Katika kongamano la Siku ya Ushirika Duniani mmejadili mambo mbalimbali ikiwemo Mifumo ya Kodi, Stakabadhi Ghalani, matumizi ya TEHAMA na Mifumo ya Masoko, na Huduma za Fedha Pamoja na changamoto nyingi zinazowakabili Wanaushirika; lengo kuu la mijadala haya ni kuona jinsi ambavyo Ushirika unaweza kusaidia kujenga Ulimwengu Bora," amesema Dkt. Ishengoma.

Akizungumza katika Kongamano hilo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, alisema kwa sasa Serikali imejikita kuendesha Vyama vya Ushirikai katika Mifumo ya kidijitali ili kuendana na kasi itakayoviwezesha vyama kupiga hatua kwa haraka.

Dkt. Ndiege amewakumbusha Wanaushirika kuendelea kununua Hisa katika Benki ya Ushirika Kilimanjaro ili kufanikisha lengo la kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika.

Amevitaka Vyama vya Ushirika kuendelea kujenga Maghala katika Vyama vyao ili kuwawezesha na kurahisisha uuzwaji wa mazao yao, na kujenga viwanda vyao kufanikisha kuchakata mazao yao na kufikia mafanikio makubwa kwenye Sekta ya Kilimo.

Akizungumza katika Kongamano hilo, kuelekea Siku ya SENSA mwezi Agosti 2022, Kamishna wa SENSA na Spika Mstaafu, Mhe. Anna Makinda, aliwahimiza Wanaushirika kushiriki kikamilifu katika zoezi Sensa ili kusaidia Serikali kujua Idadi ya watu wake ili kuwezesha kupanga Bajeti ya Taifa kwa usahihi.

## WANAHISA KCBL WATAKIWA KUONGEZA UWEKEZAJI

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika –Udhibiti Collins Nyakunga, amewataka Wanahisa wa Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) kuongeza uwekezaji kwenye Benki hiyo ili kukuza mtaji wake.

Akizungumza katika mkutano huo wa Wanahisa, Bw. Nyakunga kwa niaba ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) Dkt. Benson Ndiege, amewataka Wanaushirika kuongeza kasi ya uwekezaji katika benki hiyo ya Ushirika ili kutimiza malengo waliyojiwekea.




*Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika - Udhibiti, Collins Nyakunga, Akizungumza kwenye mkutano wa Wanahisa wa KCBL*

"Vyama vya Ushirika vitekeleze majukumu yake ili kukuza mtaji wa benki KCBL, na pia viongozi mkawe mabalozi wa benki hii katika vyama vyenu kuwa hii ni benki ya kitaifa ya ushirika," alisema Nyakunga

Aidha, Naibu Mrajis ameitaka Benki ya CRDB





kuendelea kuisaidia Benki ya Ushirika katika usimamizi wa shughuli zake wakati Benki ikiendelea kuajiri watendaji wapya ambao watasimamia benki japo imebakiza muda mchache, sambamba na hilo pia amesisitiza na kuiomba benki hiyo kuongeza mtaji.

Naye mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Ushirika Dkt. Gervas Machimu amesema kuwa, KCBL imepanga mkakati wa kuongeza mtaji wake kufikia Shilingi billioni 6.7 kutoka kwenye Vyama vya Ushirika kupitia katika vyama vikuu (UNION).




*Mwenyekiti wa Bodi ya KCBL, Dkt. Gervas Machimu akizungumza kwenye kikao cha Wanahisa*

## TCDC KUIMARISHA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA SACCOS

Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeandaa Taarifa ya Utendaji wa SACCOS kwa mwaka 2021 (The SACCOS Annual Performance Report 2021) yenye lengo la kupima utendaji wa shughuli za SACCOS kwa mwaka 2021, na taarifa hii itakuwa inaandaliwa kila mwaka.

Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amesema hayo wakati akifungua kikao kazi cha kujadili Usimamizi na Uendeshaji wa SACCOS kilichofanyika tarehe 23/09/2022 katika Ukumbi wa Ngome Holding Jijini Dar es Salaam.



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo (TCDC) Dkt Benson Ndiege akizungumza katika kikao kazi cha kujadili Usimamizi na Uendeshaji wa SACCOS*

Dkt. Ndiege amesema Mkakati huu utasaidia SACCOS kuweka mipango yenye ufanisi yanayopimika katika utekelezaji wa shughuli za Chama ili kufikia malengo waliyojiwekea.

"SACCOS zinaendeshwa kwa kuzingatia Mifumo iliyowekwa, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mingine inayotolewa kwa Maendeleo ya SACCOS nchini, na hii inapelekea Vyama kuendelea kusajiliwa na kukua kwa kasi zaidi," amesema Dkt. Ndiege.

Alisisitiza kuwa ni jukumu la Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuendelea kusimamia na kuhamasisha Maendeleo ya Ushirika ili kuondoa taswira mbaya iliyojengeka kwa jamii kuwa Ushirika haufai kwa

kuweka mifumo thabiti na kuonesha manufaa ya Vyama vya Ushirika kupitia mafanikio na masuala mazuri yanayofanyika ndani ya Sekta ya Ushirika.

"Ushirika husaidia wanachama kuinua uchumi wao na kujiendeleza kwa masuala ya Maendeleo kama vile kusomesha, kujenga na kuanzisha biashara," alisema Dkt. Ndiege.



*Viongozi SACCOS wakiwa katika kikao cha kujadili Usimamizi na Uendeshaji wa SACCOS*

Vilevile Mrajis alisema kuwa ni wakati wa SACCOS zote nchini kuanzisha Mfuko wa Kinga za Akiba na Amana. Mfuko huo utakuwa na faida kwa wanachama wote na endapo SACCOS ikishindwa kujiendesha Mfuko huo utasaidia kuwalipa wanachama fedha ambazo walizoweka kwenye SACCOS. Hivyo aliwataka washiriki kujadiliana na kutoa maoni juu ya uanzishwaji wa Mfuko huo.

Pia, amewataka Viongozi wa SACCOS kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali iliyotolewa na Mrajis ili kuweza kufikia malengo waliyojiwekea.

Dkt. Ndiege aliwasisitiza Wanaushirika kuwa wakifanya kazi kwa kufuata miongozo na kwa uwazi Vyama vitafanikiwa katika nyanja zote na kujibu mahitaji ya wanachama wao.

Aidha, Mrajis amezitaka SACCOS zote na Wadau wa Maendeleo ya Ushirika kuendelea kununua Hisa katika Benki ya Ushirika ya KCBL itakasaidia kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika (NBCT) ambayo itasaidia kuimarisha Sekta ya Ushirika ikiwemo Ushirika wa SACCOS.

## ELCT ND SACCOS KUZINDUA MATUMIZI YA KADI ZA 'ATM NA MOBILE BANKING'

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo ELCT ND SACCOS hivi karibuni kitazindua utoaji wa huduma kwa Wanachama kupitia TEHAMA ikiwemo 'Mobile Banking na ATM.'

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Collins Nyakunga, amekutana na Viongozi wa Bodi ya ELCT ND SACCOS na kukabidhi kadi za ATM kwa baadhi ya Wajumbe wa Bodi na Watendaji ambazo ziko tayari kwa matumizi, ambazo zitaanza kutumika kama majaribio.



*Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Collins Nyakunga, akimkabidhi kiongozi wa Bodi ya ELCT ND SACCOS kadi ya ATM.*

Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika alikutana na Viongozi wa Chama cha ELCT ND SACCOS tarehe 30 Julai 2022 Mjini Moshi kwa lengo la kujionea bidhaa na huduma mbalimbali zitolewazo na Chama hicho.

Bwana Nyakunga alifanya mazungumzo na Bodi ya Chama na kujadili mambo kadhaa yanayoleta tija katika utoaji wa huduma kwa Wanachama na kuwasisitiza kufanya kazi kwa maslahi ya wanachama wao.

"Bila wanachama wenu ELCT ND SACCOS si kitu, na hamuwezi kufanya jambo lolote la maendeleo hivyo wasikilizeni nini wanataka na muwahudumie kwa kufuata taratibu na kwa uharaka.

Amesema Naibu Mrajis sasa ni zama za kidigitali na anafurahishwa jinsi ELCT ND SACCOS inavyofanya kazi kwa kuangalia mbele hili jambo ni jema na SACCOS nyingine wafanye wajifunze na waige nini wanayofanya ELCT ND SACCOS.

"Si dhambi wala vibaya mtu kuiga mazuri ya mwenzie hili ni jambo jema igeni kwa manufaa ya SACCOS zenu na wanachama wa ELCT ND SACCOS mjitahidi kwendana na kasi ya viongozi wenu na mpokee mabadiliko haya kwa mikono miwili ili mzidi kuikuza SACCOS yenu," amesema Nyakunga.



*Viongozi wa Bodi ya ELCT ND SACCOS wakionesha kadi za ATM walizokabidhiwa na Naibu Mrajis Collins Nyakunga.*

## VYAMA VYA USHIRIKA KUSAJILIWA KIDIGITALI

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) inatarajia kuanza kutumia Mfumo wa kielekroniki katika kusajili wanachama katika vyama vya ushirika ili kudhibiti na kuongeza uwazi katika usimamizi wa vyama vya ushirika na kuondoa changamoto ya Usimamizi katika Vyama vya Ushirika Nchini.

Hayo yamebainishwa Jijini Dodoma Agosti 03, 2022 kwenye Maonesho ya Nane Nane Kanda ya Kati na Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Collins Nyakunga ambapo amesema lengo la kusajili Vyama na wanachama kwa njia ya kielektroniki ni kuongeza Usimamizi kwenye vyama hivyo.

"Ushirika ni taasisi inayowanufaisha wananchi katika shughuli zao za kilimo, uvuvi na mifugo kwa kutambulika na kulinda maslahi ya wananchi kwa kuwasajili kidigitali ili mchango wao katika maendeleo ya nchi uweze kufahamika," amesema Nyakunga.

"Kulikuwa na changamoto katika kuwafikia wanachama kwenye Vyama vya Ushirika na hivyo kufanya ukaguzi kuwa mgumu maana Maafisa Ushirika waliopo sio wengi lakini sasa tutavifikia kupitia Mfumo wa kielektroniki na kuvikagua kirahisi," amesema Naibu Mrajis.



*Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Collins Nyakunga kwenye Maonesho ya Nanenane Kanda ya Kati.*

Kupitia usajili kwa njia ya TEHAMA vyama vyote vitatambulika na itakuwa rahisi kufahamu mchango wa Ushirika katika Pato la Taifa na hakutakuwa na ugumu kupata takwimu na taarifa za Ushirika.

Amesema kwenye Ushirika kuna manufaa makubwa tofauti, ni vigumu Mvuvi, Mfugaji au Mkulima kuendelea akiwa peke yake kwa kuwa hataweza kupata nguvu ya Soko la bidhaa zake.

Amebainisha kuwa awali zao la Kakao kilo moja ilikuwa inanunuliwa Shilingi 1,800 lakini mara baada ya kuanza kuuzwa kupitia Mfumo wa Ushirika, bei imepanda hadi kufika zaidi ya Shilingi 5,000.

“Miaka ya nyuma, kwenye zao la Korosho kulikuwa na udanganyifu wa vipimo na bei ilikuwa ndogo sana, lakini baada ya Mfumo wa Ushirika kuanza kutumika sasa bei ni zaidi ya Shilingi 1,600, 2,000 hadi 3,000 kwa kilo moja, haya ndio manufaa ya Ushirika” alisema Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

## KAMATI YA KITAIFA YA KURATIBU HARAMBEE YA UJENZI WA ENEO LA MRADI WA KIWANDA CHA WANAWAKE YAZINDULIWA

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania imeshiriki katika Uzinduzi wa Kamati ya Kitaifa ya kuratibu harambee ya ujenzi wa eneo la Mradi wa Kiwanda cha Wanawake Tanzania kilichoratibiwa ‘Madirisha Women Cooperative Society’ kilichofanyika katika wilaya ya Kibaha Mkoani Pwani.

Mwenyekiti wa Kamati ya kuratibu Harambee hiyo, Waziri Mstaafu, Mama Anna Abdallah, ametoa pongezi kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa namnawanavyosimamia na kuhamasisha Maendeleo ya Vyama vya Ushirika nchini.




*Mwenyekiti wa Kamati ya kuratibu Harambee, Waziri Mstaafu, Mama Anna Abdallah akizungumza kwenye Harambee ya Ujenzi wa Mradi wa Kiwanda cha Wanawake*

Aidha, Kupitia Ushirika wanawake wataweza kujikwamua kiuchumi na kijamii kama wataamua kuunganisha nguvu zao kiuchumi kupitia Ushirika na kusimamia malengo yao.

Mama Anna Abdallah, ambaye alikuwa Mgeni Rasmi ametoa pongezi hizo leo tarehe 19/09/2022 wakati wa uzinduzi wa eneo hilo ikiwa ni pamoja na kuwasisitiza washiriki kuwa Ushirika ni kama dawa ukijiunga basi unakuwa umepata tiba ya ugonjwa wako kwani husimamiwa kwa mujibu wa Sheria, taratibu na miongozo mingine.

“Chombo chochote kinachofuata Sheria katika kufanya kazi zake ni lazima kifikie malengo yake, nawashauri wanawake wote nchini kujiunga katika Vyama vya Ushirika ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao na kufikia malengo kwa wakati,” alisema Mama Anna Abdallah.

Aidha, aliendelea kusisitiza kuwa Ushirika wa Madirisha utafanikiwa zaidi kama wanachama watadumisha upendo na uzalendo katika utendaji kazi zao kwa sababu rafiki wa mwanamke ni mwanamke. “Pendaneni na aminianeni, hii ni nguzo ya mafanikio kama mkiisimamia na ninaawaamini wanaushirika wa Madirisha mtafanikiwa kujenga kiwanda na mtauza bidhaa hizo ndani na nje ya nchi.




*Kamati ya kuratibu Harambee ya Ujenzi wa Kiwanda cha Wanawake wa Madirisha wakiwa katika picha ya pamoja na wanaushirika wa Kibaha*

Naye Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, amesema Ushirika wa Madirisha ni wa kuigwa kwani kina mama hawa wameweza kuunda Ushirika na kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo zinaendelea kuzalisha bidhaa mbalimbali.

“Ushirika huu ni wakipeeke sana na sasa ni wakati wa wanawake na vijana kuwa na maono mapana na makubwa kama haya ya Madirisha na kuacha kufikiri biashara ndogo ndogo.”

Vilevile, alisema Wakinamama wengi wanafanya biashara nyingi ila hazikui hivyo sasa ni muda muafaka kwa kina mama kuingia katika uzalishaji na uuzaji kwa mfumo mkubwa kupitia Ushirika.




*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson akizungumza katika Harambee ya Ujenzi wa Kiwanda cha Madirisha cha Wanawake.*

Hata hivyo, Mrajis amesema Tume sasa ina malengo ya Kuongeza Ushiriki wa vijana na kina mama katika kuunda ushirika mbalimbali ambao Tume utaisimamia kwa kufuata utaratibu.

Mwenyekiti wa ‘Madirisha Women Cooperative Society’ aliwaeleza washiriki wa harambee kuwa Ushirika wa Madirisha wa Wanawake ulianzishwa mwaka 2020 ambapo Ushirika huo unajishughulisha na viwanda vya utengenezaji wa bidhaa mbalimbali kama vile utengenezaji wa Mlonge, Ufugaji wa Samaki, sabuni, Maziwa, Batiki, Usafi na Mazingira ,Nafaka na Lishe, Mafuta na Gesi, Mafuta ya Nazi, Asali, Viungo, Shanga na Urembo.

# CHAMA CHA USHIRIKA CHAANZISHA KIWANDA CHA KUSINDIKA MAFUTA YA ALIZETI

Chama cha Msingi cha Ushirika wa Kilimo na Masoko, Chato AMCOS kimeanzisha kiwanda cha Ushirika cha kusindika mafuta ya Alizeti (Chato AMCOS Sunflower Oil double refining factory).

Kiwanda hiki cha Wanaushirika kimeanzishwa ili kusaidia katika kuondoa tatizo la upungufu wa mafuta ya kula uliokuwa unalikabili Taifa katika miaka ya hivi karibuni.



*Katibu wa Chato AMCOS, Daudi Mahelule, akionesha na kuelezea kuhusu mitambo iliyopo katika kiwanda cha kusindika mafuta ya Alizeti kinachomilikiwa na chama hicho.*

Katibu wa Chato AMCOS, Daudi Mahelule, amesema chama hicho kimeanzisha kiwanda hicho ambacho kitakuwa kinazalisha mafuta ya Alizeti inayolimwa Tanzania na kitasaidia kuleta ajira kwa Wananchi. Bwana Mahelule amesema kupitia kiwanda hicho vijana na wanawake wamepata ajira mbalimbali ambazo zitawasaidia kuongeza kipato katika maisha yao ya kila siku pia itasaidia kupunguza wimbi la vijana wazururaji.

Aidha amesema chama hicho pia kimenunua lori la mizigo, trekta na kujenga ghala la kuhifadhia nafaka kutokana na fedha za ushuru walizokusanya, na mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).




*Katibu wa Chato AMCOS, Daudi Mahelule, akionesha mafuta ya Alizeti wanayotengenezwa kwenye kiwanda hicho.*

"Ununuzi wa zana hizi za kilimo umeongeza uzalishaji na kuwapatia wananchi unafuu wa upatikanaji wa mafuta ya kula, kulimiwa mashamba na kusomba mizigo pamoja na kuwapatia ajira," alisema Katibu wa Chato AMCOS, Daudi Mahelule.

Ameeleza Bwana Mahelule kuwa ununuzi wa lori hilo utasaidia kupunguza gharama za undeshaji wa kiwanda kwasababu litatumika katika kubebea mazao kupeleka kiwandani na kubebea mafuta kutoka kiwandani kwenda sokoni.



*Katibu wa Chato AMCOS akiwa anaelezea namna mitambo iliyopo katika kiwanda cha kusindika mafuta ya Alizeti inavyofanya kazi.*





# TUNDURU WAKUSANYA UFUTA TANI 2,300 KUPITIA STAKABADHI GHALANI

Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma imefanikiwa kukusanya ufuta zaidi ya tani 2,300 kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Hayo yamesemwa na Meneja wa Ghala la Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru (TAMCU) Sarah Chirwo wakati anatoa taarifa ya ununuzi wa ufuta kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Asangye Bangu, mjini Tunduru.

Amesema tani zilizonunuliwa hadi kufikia Julai 16 mwaka huu na kwamba ukusanyaji wa ufuta bado unaendelea kwa kasi kubwa ambapo wakulima wanafurahia mfumo huo kwa sababu wanauza mazao yao kwa bei nzuri.



*Meneja wa Ghala la Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru (TAMCU), Sarah Chirwo wakati akitoa taarifa ya ununuzi wa Ufuta kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala*

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Tunduru, Musa Manjaule amesema wakulima wa Tunduru wameona faida za Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ambao umemaliza kero ya muda mrefu ya kuibiwa kupitia mfumo holela wa kununua mazao.

"Sisi Tunduru ukituambia stakabadhi tuitoe hatuwezi kukuelewa, kwa sababu tunajua ubaya wa Mfumo holela wa kununua mazao"alisema Manjaule.

Kwa upande wake mkulima, Rajabu Mohamed, mkazi wa Ligunga Tunduru, alisema "licha ya kujitokeza wakati fulani changamoto ya kuchelewa malipo, bado Mfumo wa Stakabadhi Ghalani una faida nyingi kuliko hasara".



*Ufuta ukiwa ndani ya vifungashio kwenye ghala la Tunduru*

Akizungumza baada ya kusikiliza kero za wakulima Wilayani Tunduru, Mkurugenzi wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Asangye Bangu, ameahidi kushughulikia changamoto hizo ikiwemo ya kuchelewa kwa malipo na pembejeo za kilimo.

Katika ziara hiyo Mkurugenzi wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala aliongozana na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Ruvuma, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu toka Wakala wa Vipimo na Mwakilishi wa Taasisi ya Utafiti wa Mazao - TARI.

## VYAMA VIKUU VYA USHIRIKA VYA MIKOA YA SHINYANGA NA GEITA VYAISHUKURU SERIKALI KUFUFUA VIWANDA VYA PAMBA

Vyama Vikuu vya Ushirika katika mikoa ya Shinyanga na Geita vimeishukuru Serikali kwa uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (Tanzania Agricultural Development Bank – TADB) ambayo imevipa mikopo kufufua viwanda vya kuchambua pamba ambavyo vilikuwa vimesimama kwa miaka mingi, na sasa vinafanya kazi ya kununua na kuchambua pamba kutoka kwa wakulima wa maeneo hayo na mikoa jirani kupitia vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS).

Wakizungumza kwa nyakati tofauti hivi karibuni, Viongozi wa Vyama Vikuu vya Ushirika wamesema Benki ya TADB imeleta furaha kwa wakulima wa zao la pamba kwani mazao yao yananunuliwa na uchambuzi wa pamba unaendelea kwenye viwanda vyao.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mbogwe na Bukombe (Mbogwe & Bukombe Cooperative Union – MBCU), Benedicto Bulugu amesema Serikali inavithamini na kuvipa kipaumbele Vyama Vikuu vya Ushirika ndiyo maana kupitia Benki ya TADB imewezesha upatikanaji wa mikopo ili kufufua viwanda vya kuchambua pamba vilivyokuwa havifanyi kazi



*Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Mbogwe na Bukombe (Mbogwe & Bukombe Co operative Union – MBCU), Benedicto Bulugu akizungumza na kuonesha Pamba katika kiwanda hicho.*

"Serikali inatuthamini imewezesha upatikanaji wa fedha kupitia TADB, na kwa kweli benki hii imekuwa bega kwa bega na sisi kwani wanatushauri, wanatuamini na wanatupatia fedha kwa wakati na wanachama wetu pamoja na wakulima kwa ujumla wamepata hamasa kubwa ya kuendelea kulima pamba kwani uhakika wa pamba yao kununuliwa upo," amesema Bulugu.

"Hivi sasa ile dhana ya Dhahabu nyeupe imerejea kwa kishindo, pamba ina thamani na bei imeongezeka. Hali kadhalika pamba inayozalishwa ina ubora mkubwa na wananchi hawachafui tena pamba kama zamani kwa kuweka maji, mchanga, mawe na vitu vingine, wameridhika na bei ya pamba," alieleza Bulugu.

Alisema msimu huu mwamko kwa wakulima wa Pamba umeongezeka na wamekusanya Pamba kutoka kwenye AMCOS 87 zenye wakulima 12,000 kutoka Mkoa wa Geita na mikoa jirani ikiwemo Kigoma, Mwanza na Shinyanga.

Bulugu alitumia fursa hiyo kuiomba Serikali kuwahisha pembejeo kwa ajili ya kilimo cha msimu ujao hasa mbegu na viuatilifu kwani mdudu 'Chawajani' anashambulia mmea ukiwa mdogo hivyo ni vyema maandalizi ya kukabiliana na mdudu huyo yafanyike mapema kwa kuleta viuatilifu vinavyoua wadudu hao na wakulima wapewe kwa wakati.



*Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mbogwe na Bukombe (Mbogwe & Bukombe Co operative Union – MBCU), Benedicto Bulugu akieleza namna mchakato wa kuchambua Pamba unavyokuwa.*

Naye Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Chato (Chato Co operative Union – CCU), Gereoni Gervas Chandika amesema mkopo kutoka Benki ya TADB umewezesha kufufuliwa kwa kiwanda chao ambacho hapo awali walikuwa wanakikodisha kwa watu binafsi.

"Hivi sasa ununuzi na uchambuaji wa Pamba unaendelea kwani fedha zipo na wanaendelea kusomba pamba na kulipa madeni kwenye vyama vya msingi (AMCOS) walikonunulia pamba zoezi ambalo litahitimishwa ndani ya wiki mbili na kisha kuendelea na ununuzi wa pamba kwa bei itakayokuwepo ambayo haitapungua kwa bei elekezi ya serikali shilingi 1560 kwa kilo moja ya pamba," alisema Chandika.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Khamis Majogolo alisema baada ya kufufua kiwanda chao kupitia Mkopo wa Benki ya TADB , wanaendelea kununua na kuchambua pamba huku akibainisha kuwa mwaka huu wamepata Pamba safi zaidi kutokana na maandalizi mazuri ya pamba kupitia vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS).

Vyama Vikuu vya Ushirika vya mikoa ya Shinyanga na Geita vilisema vinaendelea na mipango yake ya kuanzisha viwanda vya kusindika mafuta ya pamba kwani wamechambua mbegu za kutosha ili kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa mafuta ya kula nchini.



*Kazi ya kujaza pamba kwenye viroba ikiendelea kwenye kiwanda cha kuchambua Pamba cha Chama Kikuu cha Ushirika Mbogwe na Bukombe.*

## USHIRIKI WA TCDC KATIKA MAONESHO YA BIASHARA YA AFRIKA MASHARIKI

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imeshiriki maonesho ya 16 ya Biashara ya Afrika Mashariki kwa mara ya kwanza yaliyofanyika Jijini Mwanza kuanzia tarehe 27/08/2021 hadi 05/09/2021.



*Baadhi ya wananchi waliotembelea banda la Ushirika katika Maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki.*

Maonesho hayo yamehudhuriwa na makampuni binafsi, taasisi mbalimbali za serikali na wajasiriamali kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania katika maonyesho hayo imeshirikiana na baadhi ya wadau wake kama vile Chama Kikuu Cha Ushirika Karagwe (Karagwe District Cooperative Union - KDCU Ltd) kinachojishughulisha na uzalishaji na uuzaji wa zao la kahawa ndani na nje ya Tanzania, FSA Mkolani SACCOS Ltd kinachojihusisha na utoaji wa Mikopo kwa wanachama wake waliopo Mkoani Mwanza na Singida Youth Entrepreneurs and Consultants Cooperative Society (SIBEYECCOS) Ltd kinachojihusisha na shughuli za ufugaji nyuki na usindikaji wa asali mbichi na zenye ubora wa hali ya juu.




*Banda la Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika Maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki.*

Vyama hivyo vilivyoshiriki vimetumia maonesho haya ya 16 ya biashara ya Afrika Mashariki kuelezea huduma na bidhaa wanazozitoa pamoja na kutangaza fursa za Uwekezaji na Masoko yanayopatikana kwenye Vyama vyao.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania iliweza kuwafikia washiriki 312 walioweza kutembelea Banda kwa ajili ya kupata Elimu kuhusu dhana ya Ushirika na manufaa yake. Pia Tume imeweza kutoa elimu kwa taasisi mbalimbali ikiwemo TCCIA, TanTrade na BRELA.

Taasisi zilizotembelea banda la 'Ushirika' zimeweza kuona mchango na nafasi ya sekta ya ushirika katika ukuaji wa biashara nchini na hivyo kuahidi ushirikiano kati ya taasisi hizi ili kuleta maendeleo ya biashara katika Vyama vya Ushirika na nchini kwa ujumla.

## TCDC YASHIRIKI MAONESHO YA 46 YA KIMATAIFA YA BIASHARA

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imeshiriki Maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara yaliyoanza rasmi tarehe 28 Juni, 2022 hadi 13 Julai, 2022.

Kupitia Maonesho hayo yanayoendelea ndani ya viwanja wa Mwl Julius K. Nyerere maarufu SABASABA, Tume imeandaa Kijiji cha Ushirika kwa ajili ya wadau wake ikiwemo Vyama vya Ushirika, Wafanyabiashara na wajasiriamali mbalimbali kwa ajili ya kuonesha bidhaa na huduma mbalimbali wanazotoa, kufanya Biashara na kutangaza fursa za uwekezaji katika maeneo yao ya Uzalishaji.



*Mrajis Msaidizi wa vyama vya Ushirika Mkoa wa Dar es Salaam, Abdillah Mutabazi, akitoa maelezo kwa Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege katika Maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara, Jijini Dar es Salaam*

Vyama vya Ushirika vilivyoshiriki kwenye maonesho hayo ni pamoja na Ushirika wa Viwanda Vidogo Vidogo Dar es Salaam (DASICO), WAT SACCOS, Chama Kikuu cha Ushirika RUNALI, WETCU LTD, Chama Kikuu Cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga (SHIRECU LTD), MADIRISHA Women Cooperative Society, Chama cha Ushirika cha Msingi IGALE na Chama cha Ushirika cha Msingi IYULA.

Wengine walioshiriki pamoja na TCDC ni Wadau wanaofanya shughuli zao kupitia Ushirika na wajasiriamali wanaotokana na Vyama vya Ushirika.

Kupitia Maonesho hayo Vyama vya Ushirika vilitangaza bidhaa wanazozalisha, huduma wanazotoa na fursa za uwekezaji kwa wadau mbalimbali walioshiriki Maonesho hayo



*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt Benson Ndiege, akipata maealezo kutoka kwa Washiriki wa Maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara kwenye "Kijiji cha Ushirika"*

Julai 06, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege alitembelea Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika katika viwanja vya Mwl Julius K. Nyerere na kuvisisitiza Vyama vya Ushirika vilivyoshiriki kuongeza wigo katika uzalishaji kutegemeana na mahitaji ya soko ikiwa ni pamoja na kutambua fursa zinazopatikana kwa ajili ya kukuza Uchumi wa Vyama na wanachama wake.

"Ni vyema kwa kipindi kijacho, Kijiji cha Ushirika kikawa na wadau wake muhimu ikiwemo wajasiriamali na wafanyabiashara wanaotokana na Vyama vya Ushirika," alisema Dkt Ndiege.




*Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege akitembelea Maonesho ya Kimataifa ya Biashara.*

## MAFANIKIO YA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA CHA KAHAMA (KACU)

**Utangulizi**
Chama kikuu cha Ushirika cha Kahama (KACU) LTD kiliandikishwa tarehe 20.04.1994 chini ya sheria ya Vyama vya Ushirika namba 15 ya mwaka 1991 fungu la 30 kwa usajili namba 5493.

KACU LTD ina jumla ya wanachama 124 ambapo vyama vya ushirika vya msingi 45 vinajishughulisha na kilimo cha zao la tumbaku, Vyama 65 zao la pamba na Vyama 14 vinajishughulisha na mazao yote mawili ya pamba na tumbaku. Vyama vya msingi ambavyo ni wanachama wa KACU LTD vina jumla ya wanachama 13,655






**Dhumuni Kuu**
Kustawisha hali ya uchumi ya wanachama kwa kufanya mipango ya kuendeleza shughuli za kilimo cha zao la tumbaku, pamba na mazao mengine zinazoendeshwa na wazalishaji wanachama waliopo kwenye Vyama vilivyojiunga na KACU LTD.

**Dira ya Chama:** KACU LTD kuwa Chama kikuu cha Ushirika kinachotoa usimamizi madhubuti na weledi katika Vyama wanachama na jamii ili kuboresha viwango vya kiuchumi vya wakulima na maendeleo ya jamii katika mji wa Kahama. **Dhima ya Chama:** Kuboresha uzalishaji wa mazao miongoni mwa Vyama wanachama kwa kutoa mafunzo endelevu kwa ajili ya uendeshaji mahiri wa KACU LTD na vyama wanachama wake.

**Hali ya Uanachama na Muundo wa Kiuongozi Uliopo**
Kwa sasa KACU LTD ina jumla ya wanachama 124 ambapo vyama 45 vinajishughulisha na kilimo cha zao la tumbaku, Vyama 65 zao la Tumbaku Pia as ndio mzao yao Makuu

**Muundo wa Uongozi wa KACU LTD**




KACU LTD inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria ya Vyama vya Ushirika Na 6 ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015 pamoja na masharti ya Chama yaliyowekwa. KACU LTD imekuwa ikiwashirikisha wanachama wake katika kufanya maamuzi mbalimbali kupitia mikutano mikuu ya kila mwaka ambapo hujadili shughuli zote zilizotekelezwa kwa mwaka uliopita na kupanga shughuli za mwaka unaofuata. Watendaji wakuu wa KACU LTD wamekuwa wakiishauri Bodi ya KACU LTD juu ya namna bora ya uendeshaji wa shughuli za Chama na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwenye vikao vya Bodi ambavyo hufanyika katika kila robo ya mwaka.

Bodi ya KACU LTD imekuwa ikipokea ushauri na mapendekezo kutoka kwa watendaji na kuyafanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuwasilisha kwa wanachama kupitia mikutano mikuu kwa ajili ya maamuzi.

**Huduma za kibiashara na Uwekezaji**

KACU LTD imewekeza katika kiwanda cha kuchambua pamba kilichopo katika ofisi zake zilizopo Mtaa wa Mhongolo Kahama mjini Mkoani Shinyanga.

Kiwanda hiki kina uwezo wa kuzalisha robota 25 kwa kila mashine moja kwa masaa 8 ambapo kwa masaa 24 jumla ya robota 180 zinazalishwa zenye wastani wa kilo 181 kwa robota kwa jumla ya vyerehani 24 vilivyopo.

Uzalishaji wa robota za pamba nyuzi uliotajwa hapo juu wa robota 180 hutegemea zaidi na pamba mbegu iliyonunuliwa kwa maana ya kiwango cha uchafu uliopo kwenye pamba mbegu.

Katika msimu wa 2019/2020, KACU LTD ilinunua jumla ya kilo 2,273,663 za pamba mbegu ambapo tuliweza kuzalisha jumla ya robota 4,671 za pamba nyuzi zenye uzito wa kilo 853,362 na mbegu jumla ya kilo 1,321,080

Kwa msimu wa 2020/2021, KACU LTD ilinunua jumla ya kilo 3,469,872 za pamba mbegu ambapo tulifanikiwa kuzalisha jumla ya robota 7,108 zenye uzito wa kilo 1,326,208 na mbegu kilo 1,924,560

Aidha katika msimu wa 2019/2020, KACU LTD ilifanikiwa kulipa malipo ya pili kwa wakulima wa pamba kiasi cha Tshs 90,946,520/=

Katika misimu yote miwili, KACU LTD imefanikiwa kulipa mikopo yote ya fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kiasi cha Shilingi 3,277,606,432/= (Bilioni tatu milioni mia mbili sabini na saba mia sita na sita elfu mia nne thelathini na mbili tu) kwa msimu 2019/2020 na kiasi cha Tshs 4,972,318,200/= (bilioni nne milioni tisa sabini na mbili mia tatu kumi na nane elfu na mia mbili tu) kwa msimu 2020/2021 na kufanya jumla ya Shilingi 8,249,924,632/= (Bilioni nane milioni mia mbili arobaini na tis amia tisa ishirini nan ne elfu mia sita thelathini na mbili tu)

**Hatua tunazopitia kupanga uwekezaji wenye tija**

Ili kuhakikisha uwekezaji wetu unakuwa na mafanikio, KACU LTD imepitia hatua kadhaa kama ilivyoelezewa hapo chini.

Bodi ya KACU LTD katika vikao vyake ilipendekeza kufufua kiwanda chake cha kuchakata Pamba ambapo pendekezo hili lilipelekwa kwenye mkutano mkuu wa wanachama ambao walikubaliana na pendekezo hili na kuazimia kuomba ukomo wa madeni kwa Mrajis wa vyama vya Ushirika.

Ukomo wa madeni ulitolewa na Mrajis wa vyama vya Ushirika na ndipo KACU LTD iliomba mkopo kutoka benki ya maendeleo ya kilimo (TADB) kwa ajili ya ukarabati wa kiwanda pamoja na mtaji wa kuendesha mradi wa kuchakata pamba.

**Ushiriki wa wanachama**

Maeneo ambayo wanachama wameshiriki na Bodi ni kama ifuatavyo:

Katika kipindi cha misimu miwili (2019/2020 na 2020/2021) Mitaji ya kugharamia uwekezaji katika kiwanda cha kuchakata pamba imetokana na mikopo ya fedha kutoka benki ya maendeleo ya kilimo Tanzania (TADB) kupitia mpango wa serikali wa kufufua viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika vilivyokuwa havizalishi.

KACU LTD imekuwa na mahusiano mazuri na asasi nyingine kwa mfano mabenki, ili kufanikisha masuala ya uwekezaji kwa kufuata taratibu sahihi za uombaji wa mikopo ya fedha kwa kuwasilisha nyaraka zinazohitajika kwa wakati na kuonesha usimamizi bora wa rasilimali zinazotokana na mikopo ya fedha kutoka benki.

**8. Manufaa ya uwekezaji kwa Wanachama**

Bei nzuri ya pamba: Kupitia uwekezaji uliofanywa na KACU LTD, wanachama (wakulima wa pamba) wananufaika kupitia bei inayotolewa na KACU LTD wakati wa ununuzi.

KACU LTD imekuwa ikiongeza bei ya kununulia pamba kutoka kwa wakulima ikilinganisha na bei ya pamba nyuzi iliyopo kwenye soko la dunia.

Huduma kwa wakulima wa tumbaku: Kwa upande wa wanachama wanaojishughulisha na kilimo cha zao la tumbaku wamekuwa wakinufaika kutokana na uwekezaji wa kiwanda cha kuchambua pamba kwa kupata huduma mbalimbali ikiwemo usimamizi unaowezeshwa na mapato yatokanayo na uwekezaji wa kiwanda.

Ununuzi wa magari: KACU LTD imeweza kununua magari mawili aina ya Land Cruiser kutokana na uwekezaji ilioufanya, ili kurahisisha utendaji wa shughuli za kila siku za Chama kwa wanachama wake.

**9. Mipango ya baadaye**

Chama chetu kina mpango wa kununua na kusimika mashine ya kukamua mafuta yatakayotokana na mbegu za pamba baada ya kuchambuliwa lakini pia mashine hizo zitakuwa na uwezo wa kukamua mafuta yatakayotokana na mazao ya alizeti, karanga na aina zingine za mbegu za mafuta kwa mfano ufuta.

## *HAI RURAL TEACHERS SACCOS WATOA MISAADA KWA KITUO CHA WATOTO CHA NEEMA*

Wanaushirika wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (HAI RURAL TEACHERS SACCOS - HRT) walitembelea na kutoa misaada kwa Kituo cha watoto cha NEEMA kilichopo Kalali, Machame - Hai, Kilimanjaro.

Wanaushirika hao waliongozwa na Mwenyekiti wao, Mwalimu Alex Warioba, katika kutekeleza Msingi wa Ushirika wa Kuijali Jamii ambapo HRT SACCOS imejiwekea utaratibu wa kushirikiana na jamii kila mwaka.

wenyekiti alisema chama kimetoa Shilingi 1,500,000 pamoja na mahitaji mengine yenye thamani ya Shilingi 500,000 kwa lengo la kusaidia watoto wenye uhitaji waliopo katika kituo hicho.



*Wanaushirika wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (HAI RURAL TEACHERS SACCOS – HRT walipotembelea na kutoa misaada kwa Kituo cha Watoto cha NEEMA kilichopo Kalali, Machame - Hai, Kilimanjaro.*

Aliendelea kusema Mwalimu Alex kuwa kituo cha Neema kina watoto 52 wenye umri wa kuanzia siku moja na kuendelea. Watoto hawa wamepatikana katika mazingira tofauti tofauti.

"Watoto wa hapa wapo waliookotwa inamaana wametupwa na wazazi wao wakiwa na siku 1, wapo ambao wazazi wao walifariki wakati wa kujifungua, yupo mmoja ana utapiamlo, wazazi wake walikuwa wanamnywesha pombe, wanampiga, ana miezi 9 kwa sasa", amesema Mwalimu Alex.

Vilevile ameiaomba jamii kukemea vikali vitendo vya ukatili kwa wototo, na wajitahidi kupanga uzazi pale wanapoona hawana uwezo wa kulea mtoto au hawapo tayari, zaidi wawe na Hofu ya Mungu na kukumbuka mtoto wa mwenzio naye ni wako.



*Wanaushirika wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (HAI RURAL TEACHERS SACCOS – HRT) wakiwa katika picha ya pamoja na watoto na viongozi wa kituo NEEMA.*

## VYAMA VYA USHIRIKA MKOANI DODOMA VYATOA MISAADA

Vyama vya Ushirika mkoani Dodoma vimetoa misaada katika vituo vya kulelea watoto na wazee vya Jijini Dodoma vya Hombolo na Kisidet pamoja na Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu mkoani Dodoma.



*Watoto wakiwana na nyuso za furaha baadaya kukadiwa vitumbalimbali vilivyotolewa na Vyama vya Ushirika mkoani Dodoma.*

Misaada hiyo imetolewa na Vyama hivyo kwa lengo la kutimiza Msingi wa saba wa Ushirika wa Kuijali Jamii, ambapo Kaimu Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Dodoma, Octavian Bidyanguze, amevipongeza Vyama vilivyojitokeza kutoa sehemu ya mapato ya Vyama hivyo kwa Wazee na Watoto walioko katika vituo vya kulelea na kuwahifadhi wazee.

Bidyanguze amevihamasisha Vyama vya Ushirika kuendelea kutoa misaada ili kutekeleza Msingi wa Ushirika unaohimiza Vyama vya Ushirika kutoa Misaada kwa watu wenye uhitaji.



*Wanaushirika waliotoa misaada katika vituo vya kulelea Watoto wenye mahitaji maalum na Wazee mkoani Dodoma wakimsikiliza mmoja wa waratibu wa vituo hivyo.*

Amesema vyama vyote vya ushirika nchini vikiwa na tabia ya kutoa msaada kwa watu wenye uhitaji itasaidia watu hao kupata mahitaji wanayoyahitaji kwa urahisi zaid hivyo ni wajibu wa vyama vya ushirika kufanya jambo hilo jema kila inapoitajika.

Vyama vilivyotoa misaada ni pamoja na UDOM SACCOS LTD , MKOMBOZI SACCOS LTD, MWASHITA SACCOS LTD, KKKT ARUSHA ROAD SACCOS LTD, TMA SACCOS LTD, CBE SACCOS LTD, MNRT SACCOS LTD, na AFYA SACCOS LTD ambavyo vimetoa Vyakula, Sabuni, Vifaa vya Usafi na Taulo za kike.



*Baadhi ya Wazee na Watoto walioko katika vituo vya kulelea watoto wenye mahitaji maalum na kutunza wazee wakisalimiana na Wanaushirika mkoani Dodoma.*

*Limetolewa na*
Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)
Mtaa wa Kuu, S. L. P. 201, DODOMA.
Simu: +255 26 23 22456, Telefax: +255 26 23 21973
B.Pepe: ushirika@ushirika.go.tz Tovuti: www.ushirika.go.tz
ushirika_tcdc Tume ya Maendeleo ya Ushirika